Jina _____ Nambari ya mtihani _____

Sahihi ya Mtahiniwa _____

Tarehe _____

Nambari usajili _____

102/1
KISWAHILI
KARATASI LA 1
INSHA
JULAI, 2011
MUDA: 1 ¾

MTIHANI WA SHULE ZA UPILI WA KUJITAYARISHIA KCSE, WILAYA YA MAKINDU
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI LA 1
INSHA
JULAI
MUDA : SAA 1 ¾

MAAGIZO
(a) Andika Insha mbili. Insha ya kwanza ni ya lazima.
(b) Kisha chagua Insha moja nyingine kutoka kwa hizo tatu zilizobakia.
(c) Kila Insha isipungue maneno 400.
(d) Kila Insha ina alama 20.

Kijitabu hiki kina kurasa 2 ambazo zimepigwa chapa

Fungua ukurasa

1. Insha ya lazima
   Andika barua ya kuomba nafasi ya kazi ya ualimu katika shule moja ya upili.
   Barua yako iandamane na wasifu kazi.

2. Mali ni sawa na maua.

3. Malizia kwa ….. usiku huo nililala unono na kuota ndoto tamu ya asali.

4. Mtoto wa kike ametengwa na mazingira kielimu.
   Jadili mikakati inayowekwa na serikali kumsaidia mwanafunzi wa kike.

102/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA
JULAI, 2011

MTIHANI WA SHULE ZA UPILI WA KUJITAYARISHIA KCSE, WILAYA YA MAKINDU
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI LA 1
INSHA
JULAI, 2011

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. Insha ya lazima
   Insha ina sehemu mbili
   Mwanafunzi aandike barua ya kuomba kazi kikamilifu kisha aandike
   Wasifu kazi kikamilifu.

2. Insha ya methali : Mali ni sawa na maua.
   M.f. Kwa kawaida maua hunyauka baada ya kuchanua kwa muda mfupi sana
   Mat. Hutumiwa kumsuta na kumtanabahisha mtu anajitapa au kuringa kwa kuwa ana mali.
   Hali hiyo inayomfanya aringe huweza kutoweka wakati wowote akabakia kibapara au fukara.

3. - Hii ni Insha ya mdokezo.
   - Ichukue mtindo wa Insha ya Masimulizi.
   - Mtahiniwa aonyeshe uwezo wa kusisimua na kuteka hisia kwa taharuki na taswira nzuri.
   - Kisa kioane vyema na mdokezo.
   - Mtahiniwa atayebadili mdokezo kwa vyovyote vile atuzwe 01 kwani huko ni kujitungia swali.
   - Kisa kioane vyema na mdokezo huu hasa na kiwe cha furaha.

4. Mwanafunzi arejelee maswala kama

   (i) Kutolewa kwa sodo shuleni.

   (ii) Kuhakikisha kuwa alama zao za kujiunga na vyuo zi chini ya zile za wenzao wavulana.

   (iii) Msaada wa serikali kupitia pesa za ustawi wa maeneo bunge zielekezwe hasa kwa elimu ya mtoto wa kike.

   (iv) Kujengewa shule nyingi za bweni ili kuwatoa kwenye kazi za nyumbani.

Jina _____ Nambari ya mtihani _____

Sahihi ya Mtahiniwa _____

Tarehe _____

Nambari usajili _____

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
JULAI, 2011
MUDA: 2 ½

MTIHANI WA SHULE ZA UPILI WA KUJITAYARISHIA KCSE, WILAYA YA MAKINDU
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI LA 2
LUGHA
JULAI , 2011
MUDA : SAA 2 ½

MAAGIZO
(a) Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(c) Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika kijitabu hiki cha maswali.
(d) Karatasi hii ina kurasa 10 zilizopigwa chapa.
(e) Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

Kwa matumizi ya mtahini pekee

SWALI	UPEO	ALAMA
	JUMLA	

Kijitabu hiki kina kurasa 11 ambazo zimepigwa chapa

Fungua ukurasa

UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.

Tutakuwa tunajidanganya tukianza kujitanua vifua na kusema kwamba Kiswahili hakina matatizo. Ni kweli kwamba Kiswahili kina hadhi kubwa kitaifa na kimataifa. Rais anaweza kuapishwa kuchukua wadhifa wake kwa Kiswahili. Mjumbe anaweza kuamka na kuhutubia kongamano la Muungano wa Afrika kwa Kiswahili. Unaweza kusoma Kiswahili kwenye mtandao wa wavuti au kukisikiliza katika idhaa za kitaifa na kimataifa. Unaweza kufundisha Kiswahili Marekani, Mariakani, Uholanzi au Uingereza. Lakini huwezi kufumbia macho matatizo chungu nzima yanayoikabili lugha hii.

Usambazaji wa lugha huenda sambamba na uwezo wa wasemaji wa lugha. Wakoloni walikuwa na uwezo mkubwa. Walikuja na lugha zao wakatushikia shokoa tuzijue na tuzitumie; tupende tusipende. Ndiyo maana Afrika inakabwa koo na Kireno na Kiarabu au lugha nyingine za wenye nguvu. Walikuwa na uwezo na walitumia mtutu wa bunduki kuhakikisha wanatusemesha lugha zao. Kwa bahati mbaya, Kiswahili hakina wasemaji wenye uwezo wa kutumia mtutu wa bunduki kuwalazimisha watu kukisema. Hatusemi kwamba Kiswahili ni lugha ya wanyonge. La hasha! Tunasema kwamba wale waitwao Waswahili sio tabaka au kabila la watu au taifa lenye uwezo wa kuwadhibiti watu wengine na kuwamezesha ustaarabu wao. Hoja hapa ni kwamba wale wasemao Kiswahili huonwa kama wanyonge.

Kuna mwelekeo mbaya sana uliokithiri unaoshikilia. Kiswahili ni lugha ya ombaomba. Hapana shaka mwelekeo huo una dosari kubwa. Lakini upo. Kutokana na hilo wapo watu wenye heshima zao na akili zao razini ambao wanaona soni kuzungumza Kiswahili. Hawataki kuonekana hawakusoma au kisomo chao ni duni. Vile vile kuna wale ambao watakisema Kiswahili lakini hawaoni aibu kuzivunja kanuni zake za kisarufi. Wanaweza kuaibikia kubananga sarufi ya Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu lakini hawana haya na ndio wanaosema kuwa Kiswahili ni pungufu na hakiwezi kufundisha masomo changamano kama vile hisabati na sayansi, kana kwamba masomo hayo ni lugha sio taaluma. Yamkini wanaandama falsafa inayosema, “Mnyonge mnyongeni.” Kama hili si tatizo labda itolewe fasili nyingine ya neno “tatizo” Kwa miaka nenda miaka rudi vyombo vya habari vimesaidia katika usambazaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa miaka nenda miaka rudi vyombo vya habari vimesaidia katika usambazaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa hadhira vyombo hivi huwa ni ruwaza na vielelezo vya ufasaha wa lugha si hoja kama ni redio, runinga au magazeti. Hata hivyo, baadhi ya vyombo vya habari vimetepetea mno kiasi kwamba vimekuwa adui mkubwa wa lugha ya Kiswahili. Inashangaza jinsi wamiliki wa vyombo hivi wanavyowapa ajira watu ambao kwa kweli umahiri wao wa lugha ya Kiswahili ni mdogo au haupo kabisa. Kuna wale waitwao wanahabari wanaohudumu katika vyombo vinavyotumia Kiswahili lakini ambao ni vielelezo vya vile Kiswahili kisivyopaswa kusemwa au kuandikwa. Hii ni tanzia kwa maendeleo ya Kiswahili. Tunadahili kwamba vyombo vya habari vinachangia katika “kukinyonga” Kiswahili.

Kwa hakika “wanyongaji” wa Kiswahili ni wengi. Miaka ya mapema ya themanini palizuka kilugha cha vijana kilichopewa jina la Sheng. Nimcheshi mmoja aliyesema urefu wa Sheng ni “Shemeji Hakuna Elimu, Gura.” Sheng ndiko walikohamia au kuguria vijana kilugha nje ya mawanda ya elimu. Walitaka kujificha kwenye kwapa za vijineno visiyoeleweka na wazazi wao. Sasa ajabu ni kwamba waliokuwa wakisema Sheng zama hizo, wenyewe wamekuwa wazazi. Na bado wanasema Sheng. Hatimaye Sheng imekuwa lugha ya taifa isiyo rasmi. Inazungumzwa nyumbani, arusini, matangani, kanisani, redioni na kuandikwa magazetini. Kwa sababu sheng “imeiba” maneno mengi kutoka kwenye Kiswahili sanifu na kuyasongoa, inakuwa taklifu kujua tofauti. Wanafunzi wanatatizika kupambanua baina ya Sheng na lugha sanifu katika insha na maandishi yao.

Ipo hatari kwamba Sheng ikishamiri sana kama inavyoendelea kushamiri, watu wachache sana wataweza kuzungumza na kuelewa Kiswahili sanifu. Kiswahili sanifu kinaweza kujikuta kimeenguliwa kutoka kwa hadhi ya lugha ya taifa hadi kuwa lugha ya kigeni. Hata pengine hilo limeanza kutokea tayari. Si ni kweli kwamba kwa baadhi ya maashiki wa Sheng Kiswahili ambacho ni Kiswahili kweli kinawatanza kama vile wanavyotanzwa na Kichina au Kiyunani? Wanapotazama habari za Kiswahili kwenye runinga wanabaki kutumbulia macho picha pasi kuelewa msamiati unaotumiwa. Kiswahili kinastahimili makuruhu mengi, na mengine hutoka vyanzo visivyotarajiwa. Asasi zinazohusika na Kiswahili pia huchangia kudorora kwa hali ya Kiswahili. Kosa kubwa lilipo ni ukosefu wa ushirikiano. Kuna ukosefu wa ushirikiano kati ya watengenezaji wa bidhaa au watoaji huduma wa matangazo ya kibiashara. Kila uchao kiwango cha Kiswahili kwenye matangazo ya kibiashara kinaendelea kudidimia.

Mathalani, unaposoma au kusikia kauli kama vile “net iliyotibiwa” kama tafsiri ya treated mosquito net, unajiuliza kama kitu kinachorejelewa kilikuwa kinaugua ugonjwa gani. Si vigumu kushuku kwamba watu wengi wanaotafsiri matangazo ya kibiashara ni malimbukeni wasiojue mbele wala nyuma ya tafsiri. Labda wapo Wakenya wengine wenye uwezo mkubwa wa tafsiri lakini ambao ushauri na uhusika wao haukutafutwa. Ukweli huu ndiyo tanzia ya lugha hii. Kuna watu waliojiambika ubingwa na kuaminiwa ni mabingwa na kupewa majukumu ambayo si kiasi chao kuyatekeleza. Tokea ni tafsiri zenye taksiri. Hili linatuleta katika swala zima la ushirikiano. Kwa sababu Kenya ina wasomi wengi waliotaalamika katika Kiswahili mbona hawashirikiani kuunda chombo mahsusi kukiendeleza Kiswahili? Ni kweli kwamba vyama kadha vimekuwa vinabuniwa na kujiita vyama vya Kiswahili, lakini aghalabu shabaha ya waasisi wa vyama hivyo ni kujifaidi wenyewe. Huu ubinafsi unahujumu juhudi za ushirikiano na asasi nyingine za ndani na nje ya nchi kukiendeleza Kiswahili.

Ni fedheha kwamba ingawa Kenya huhesabiwa kuwa nchi inayozungumza Kiswahili, wanafunzi wa kigeni wanaotaka kujifunza Kiswahili sanifu husafiri hadi Tanzania kufaidi uhondo wa Kiswahili hicho. Dar es Salaam imegeuzwa Makkah ya Kiswahili, ambako wanaokiwania wanakimbilia kuhiji. Matatizo yanayokitanza Kiswahili yasipotanzuliwa Kenya itaendelea kuwa tanbihi tu katika kurasa za matini ya lugha azizi ya Kiswahili.

Maswali

1. Taja matatizo manne yanayokumba Kiswahili. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

_____

2. Pendekeza njia nne za kuyashughulia matatizo haya. (alama 4)

_____

_____

_____

_____

_____

3. Unafikiri hoja ya mwandishi kwamba hatimaye Sheng itakuwa lugha ya taifa ni kweli? Eleza. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

_____

4. Vyombo vya habari vimechangia kiasi kikubwa kwa matatizo yanayokumba lugha ya Kiswahili. Eleza. (alama 4)

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

5. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa kwenye kifungu: (alama 3)

(a) Taksiri

_____

_____

_____

(b) Tanzia

_____

_____

_____

(c)Wakatushikia shokoa

_____

_____

_____

MUHTASARI (alama 15)
Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Sawa na jinsi binadamu alivyokuwa na idadi kuenea kutoka usuli wake, ndivyo lugha ya Kiswahili ilivyoenea. Haitishwi na matatizo mengi bali inasambaa kwingi kila uchao. Kiswahili kimesambaa sio tu katika nchi za Afrika Mashariki bali bara nzima na ulimwengu kwa jumla.
Lugha hii imepata hadhi na kuwa lugha mojawapo ya lugha kumi na mbili za dunia. Vivyo hivyo, imetwikwa majukumu katika ngazi ya kitaifa na kimataifa pia.
Kwanza watu wa makabila mbalimbali huwasiliana kwa Kiswahili, ikawa kwamba kanisani na hata vituoni vya magari utawasikia wakizungumza Kiswahili. Hali hii imedidimiza ule uhasama wa kikabila na utengamano baina ya makabila. Katika mikutano na makongamano ya kimataifa, Kiswahili hutumika sana. Kwa jinsi hii, ushirikiano wa kimataifa huimarishwa si ajabu kuwasikia Wa Asia, Waamerika na Waafrika wakiwasiliana kwa Kiswahili. Wao hujihisi wamoja kwa sababu ya kutumia lugha moja – Kiswahili.
Jumuiya ya Afrika Mashariki ilifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi. Mashirika husisitiza mawasiliano kwa lugha hiyo, hali kadhalika, umoja wa Afrika uliiga sera hiyo ya kutumia Kiswahili kama lugha rasmi. Ilikuwa fahari kubwa kuwasikia viongozi kama vile raisi Fredrick Chiluba akihutubia mkutano kwa Kiswahili.
Umoja huo umeendeleza mikutano ya kujadili mizozo mbalimbali barani humu ambapo lugha ya Kiswahili imekuwa ikitumika katika mikutano hii. Tukirejea nchini, mikutano ya viongozi imeongozwa kwa lugha ya Kiswahili. Rais wa nchi huhutubia wananchi mtungo uo huo, kueleza sera za serikali kwa wananchi. Hivyo Kiswahili hutumiwa kupatanisha serikali na wananchi wake.
Katika kufunza Kiswahili, utamaduni na maarifa ya Waafrika hupitishwa kutoka kizazi hadi kingine. Mathalan methali husheheni mengi kuhusu mila na desturi za jamii mbalimbali. Nyimbo, ngano na misemo vivyo hivyo

Mwafrika amepata fursa ya kutoa mchango wake katika ustaarabu kupitia lugha hii. Wanaisimu wapenzi wa Kiswahili wamejitahidi kukisanifisha na kukiimarisha Kiswahili kadri ulimwengu unavyokuwa kimaendeleo. Nasi hatuna budi kukitumia na kukionea fahari katika Nyanja tunazoshiriki.

Maswali

1. Fupisha aya mbili za kwanza kwa maneno (Maneno 25- 35) . (alama 6)
Matayarisho

Nakala safi

2. Eleza majukumu ya Kiswahili kwa maneno (40-50) (alama 9)
Matayarisho

Nakala safi

3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

(a) (i) Taja irabu moja ya kati na utoe sifa zake tatu. (alama 3)

(ii) Sahihisha orodha ifuatayo ya konsonanti za Kiswahili. (alama 1)
th, Z, L, P, Q, W, X, V

(b) (i) Viambishi ni nini? (alama 1)

_____

_____

_____

_____

(ii) Tenganisha kwa kuonyesha mzizi, viambishi awali na tamati. (alama 3)
Wahubiriapo

_____

_____

_____

_____

_____

_____

(c) Andika ukubwa.
Nyoka hatari wamepanda mtini. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(d) Tumia kihusishi cha kutaka heri katika sentensi. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(e) Kitenzi <u>fisha</u> ki katika kauli gani? (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(f) Andika katika wingi. (alama 2)
Mama huyo analima shamba lake.

_____

_____

_____

_____

(g) Eleza kwa kutoa mifano matumizi mawili ya mabano. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

_____

(h) Kanusha: (alama 2)

(i) Ukisoma kwa bidii, utafuzu vyema.

_____

_____

_____

_____

(ii) Gari jipya limeharibika

_____

_____

_____

_____

(i) Eleza matumizi ya ‘kwa’ katika : (alama 1)

Musa alikwenda hospitalini kwa matibbau.

_____

_____

_____

_____

(j) Tambua aina za yambwa katika: (alama 3)

Mwanafunzi alisahihishiwa Insha na mwalimu kwa kalamu.

_____

_____

_____

_____

_____

_____

(k) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo. (alama 2)

(i) Sali

_____

_____

_____

_____

(ii) La

_____

_____

_____

_____

(l) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 2)

"Lo! Siamini kuwa yule askari polisi amemuua mkubwa wake! Alisema Waziri wa usalama.

_____

_____

_____

_____

_____

(m) Changanua kwa vielelezo vya matawi. (alama 4)

Kijana mzee anakula kifisi.

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

(n) Tumia neno maadamu katika sentensi . (alama 1)

_____

_____

_____

_____

(o) Tunga sentensi ukitumia kiwakilishi cha 'a' unganifu. (alama 1)

_____

_____

_____

_____

(p) Tumia neno gani kama: (alama 2)

(i) Kivumishi

_____

_____

_____

_____

(ii) Kiwakilishi

_____

_____

_____

_____

(q) Tofautisha: (alama 2)

(i) Chakula chote kimeliwa

(ii) Chakula chochote kitaliwa

_____

_____

_____

_____

_____

(r) Eleza matumizi ya “ni” katika. (alama 1)

Ondokeni

_____

_____

_____

_____

(s) Bainisha kirai katika: (alama 1)

Tajiri mwenye duka kubwa amefariki.

_____

_____

_____

_____

SEHEMU D. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

Timu hizi zilipokutana mara ya mwisho Chui iliitinga Boga mabao matatu kwa nunge …. Madede amewahi kuvunja rekodi ya dunia mara mbili ….

(i) Hii ni sajili gani? (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(ii) Taja wahusika wawili katika mazungumzo haya. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(iii) Eleza sifa zozote sita za sajili inayorejelewa. (alama 6)

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
JULAI, 2011

MTIHANI WA SHULE ZA UPILI WA KUJITAYARISHIA KCSE, WILAYA YA MAKINDU
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI LA 2
LUGHA
JULAI, 2011

MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

Majibu ya ufahamu – Matatizo yanayokumba Kiswahili.

1. Matatizo yanayokumba Kiswahili.
   - (i) Kuwepo kwa kasumba ya kikoloni miongoni mwa baadhi ya watu kuhusu matumizi ya Kiswahili.
   - (ii) Kutowepo kwa sera madhubuti au imara kuhusu matumizi ya Kiswahili.
   - (iii) Ukosefu wa mwongozo kuhusu uendelezaji wa misamiati na istilahi za Kiswahili.
   - (iv) Kutopendelewa kwa Kiswahili kunakotokana kwa lugha nyingine kama Kiingereza, Kijerumani, Kifaransa, n.k
   - (v) Ukosefu wa wataalamu wa kutosha wa lugha ya Kiswahili.
   - (vi) Ukosefu wa wataalamu wa kutosha humaanisha kuwa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa njia ifaayo unakabiliwa na tatizo kubwa.
   - (vii) Kutokuwepo na waandishi wa kutosha wanaoandika katika lugha ya Kiswahili.
   - (viii) Kuzuka na kuenea kwa lugha ya Sheng miongoni mwa wanajamii.
   - (ix) Ukosefu wa vitabu bora vya kuwasaidia wanaojifunza lugha hii.
   - (x) Mashirika ya uchapishaji kuelekea kukipa Kiingereza kipaumbele katika uchapishaji wao.
   - (xi) Uhaba wa magazeti au majarida ya Kiswahili ambazo ni msingi muhimu wa uzambazaji wa lugha.
   - (xii) Kuendelea kutumiwa kwa lugha ya Kiingereza katika shughuli nyingi nyingi za kitaifa.
   - (xiii) Ukosefu wa chombo cha kuiendeleza lugha ya Kiswahili kama taasisi ya Kiswahili n.k.
   - (xiv) Kutokuwepo msukumo wa kutosha miongoni mwa wanasiasa au wanaopanga sera kuihusu lugha ya Kiswahili.
   - (xv) Ukosefu wa utafiti wa kutosha kuhusu tofauti za lugha ya Kiswahili.

2. Jinsi ya kuyashughulikia matatizo yanayokumba Kiswahili.
   - (i) Kutilia mkazo ufundishaji ufaao wa ya Kiswahili
   - (ii) Kuhimiza matumizi ya Kiswahili katika nyanja nyingi za maisha yetu.
   - (iii) Kupitishwa kwa sera nzuri inayoweka wazi malengo ya serikali kuihusu lugha hii na kuota mwongozo ufaao hatima (destiny) ya lugha yenyewe.
   - (iv) Kuhimiza kuwepo kwa idara za Kiswahili taasisi za juu ili kuendeleza utafiti wa Kiswahili
   - (v) Kuwepo kwa sheria ambazo zinazohimiza wazi majukumu na nafasi ya Kiswahili nchini.
   - (vi) Kubuniwa kwa vyombo vya kukiendeleza Kiswahili kama taasisi ya utafiti wa lugha hii.
   - (vii) Raia kuhamasishwa na kukumbushwa umuhimu wa kuionea fahari lugha ya Kiswahili.
   - (viii) Wachapishaji wanahimizwa kuchapisha machapisho ya lugha ya Kiswahili. Serikali inaweza kuzuka na vituo vya kuwafanya wachapishaji hao wasichelewe kuchapisha vitabu hivyo.

Kijitabu hiki kina kurasa 4 ambazo zimepigwa chapa

Fungua ukurasa

(ix) Serikali kutoa au kutenga kasima (kiasi fulani cha fedha) fulani ambayo inaweza kutumiwa kusaidia ukuzaji wa Kiswahili katika taasisi ya elimu.

(x) Kuanzishwa kwa tuzo zinazowatunza waandishi wanaoandika kazi nzuri zinazosaidia ukuzaji wa Kiswahili.

(xi) Kuhimizwa kuwepo kwa magazeti ya Kiswahili ambayo yatauzwa kwa bei inayowafanya wengi kuyamudu.

(xii) Kuifanya lugha ya Kiswahili msingi muhimu katika taasisi za elimu. Kwa mfano, daktari asiweze kuwa daktari bila kuonyesha umilisi (uwezo) mzuri wa lugha ya Kiswahili.

(xiii) Kuwepo kwa vipindi vya redio na runinga ambavyo vinahimiza matumizi fasaha ya lugha ya Kiswahili.

(xiv) Kuhimiza raia kutambua kuwa Kiswahili ni msingi muhimu wa kujitambulisha kama raia wa nchi hii.

3. La. Haiwezi kuwa lugha ya taifa kwa kuwa haina sarufi na inabadilika kila uchao. Ndio, iwapo itiatumiwa na wengi na kusambaa kwa namna ambavyo itatumiwa kwa mapana na marefu katika maisha ya jamii.

4. Vyombo vya habari na matatizo ya Kiswahili.

(i) Baadhi ya vyombo vya habari vimetepetea kwamba vimekuwa adui mkubwa wa lugha ya Kiswahili.

(ii) Baadhi ya vyombo vya habari vimewapa ajira watu ambapo umahiri wao wa lugha ya Kiswahili ni mdogo au haupo kabisa. Kuna wale waitwao wanahabari wanaohudumu katika vyombo vinavyotumia Kiswahili lakini ambao ni vielelezo vya vile Kiswahili kisivyopaswa kusemwa au kuandikwa. Hii ni tanzia kwa maendeleo ya Kiswahili. Kwa hivyo, vyombo vya habari vinachangia katika "kukinyonga" Kiswahili.

(iii) Kuna ukosefu wa ushirikiano kati ta watengezaji wa bidhaa au watoaji huduma na waundaji wa matangazo ya kibiashara. Kila uchao kiwango cha Kiswahili kwenye matangazo ya kibiashara kinaendelea kudidimia.

(iv) Tafsiri zipatikanazo katika vyombo vya habari ni za hali yachini na zinazodunisha hadhi ya Kiswahili na kukikoroga. Si vigumu kushuku kwamba watu wengi wanaotafsiri matangazo ya kibiashara ni malimbukeni wasiojua mbele wala nyuma ya tafsiri.

5. (i) Taksiri – kuwa na walakini, makosa.
(ii) Tanzia – ukweli mbaya au mchungu.
(iii) Wakatushikia shokoa – wakatulazimisha tuzijue.

MAJIBU YA UFUPISHO

Ufupisho

(a) Kiswahili kimeenea kote ulimwengu kote kadri binadamu anavyozidi kuenea. Kutoka usuli wake kimejumuishwa katika lugha kumi na mbili za dunia hivyo kupewa jukumu la kitaifa na kimataifa (alama 5, moja utiririko)

(b) Mawasiliano baina ya makabila mjini.
- Lugha rasmi katika Afrika Mashariki na umoja wa Afrika
- Kusuluhisha mizozo baina ya nchi.
- Kupatanisha serikali na mwananchi.
- Kueleza utamaduni wa watu.

(alama 10, moja ya utiririko)

3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

(a) (i) a
Sifa
Hutamkwa midomo ikitandazwa
Inapotamkwa hewa hazuiliwi katika ala zozote.
(ii) Q, na X hazipatikani katika alfabeti ya Kiswahili.

(b) (i) Ni viungo vyenye maana ya kisarufi ambavyo huambatanishwa na mzizi wa neno ili kulipa neno maana mbailimbali.

(ii) Wa – hubiri – a – po
kiambishi mzizi viambishi
awali tamati

(c) Ukubwa
Majoka hatari yamepanda majitini.

(d) Mifano.
Inshallah, Afya
Asanteni
Basi

(e) Kutendesha

(f) Wingi
Akina mama hao wanalima mashamba yao.

(g) Matumizi ya mabano
(i) Kuonyesha maneno ambayo si ya lazima katika usemi.
(ii) Kuonyesha jambo la ziada.
(iii Kuzingira nambari, hasa katika orodha mifano (a), (b).
(iv) Katika maandishi ya kitamthilia kutoa maelekezo kwa waigizaji na wasomaji.

(h) Ukanusho
(i) Usiposoma kwa bidii hutafuzu vyema au
(ii) Kama husomi kwa bidii, hutafuzu vyema.

(i) Gari jipya halijaharibika.
Matumizi ya kwa
Sababu

(j) Yambwa
Mwanafunzi alisahihishwa Insha na mwalimu
Yambwa tendewa Yambwa tendwa
Kwa kalamu
Ala

(k) Uundaji wa nomino
(i) Sali – sala
(ii) La – mlo, chakula, ulaji, malaji

(l) Usemi wa taarifa

Waziri wa usalama alimaka kuwa yule askari polisi alikuwa amemuua mkubwa wake.

(m) Uchanganuzi wa sentensi

Ni sentensi sahihi



(n) Maadam

kwa sababu

(o) La mama limepotea

Vya mwalimu vimeraruka.

(p) (i) Gari gani limeibwa?

(ii) Gari limeibwa ?

(q) (i) Chote – kwa jumla

(ii) Chochote – bila ubaguzi

(k) Kutoa amri

(s) Kirai

Mwenye duka kubwa – Kirai kivumishi

SEHEMU YA D: ISIMU JAMII (alama 10)

Timu hizi zilipokutana mara ya mwisho Chui iliitinga Boga mabao matatu kwa nunge …
Madebe amewahi kuvunja rekodi ya dunia mara mbili …..

(i) Hii ni sajili gani?

Michezo (alama 2)

(ii) Taja wahusika wawili katika mazungumzo haya.

- Mtangazaji
- Msikizaji wake (alama 2)

(iii) Eleza sifa zozote sita za sajili inayorejelewa.

- Kuchanganya ndimi
- Lugha ya mkato / kujaliza
- Lugha yenye ucheshi
- Haizingatii usanifu wa lugha.
- Matumizi ya msamiati kama mpira, bao n.k
- Utohozi wa maneno boli, golikipa, refarii n.k
- Kutozingatia msamiati halisi.

Zozote 6 x 1 = 6

Jina _____ Nambari ya mtihani _____

Sahihi ya Mtahiniwa _____

Tarehe _____

Nambari usajili _____

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
JULAI, 2011
MUDA: 2 ½

MTIHANI WA SHULE ZA UPILI WA KUJITAYARISHIA KCSE, WILAYA YA MAKINDU
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI LA 3
LUGHA
JULAI, 2011
MUDA : SAA 2 ½

MAAGIZO

(a) Jibu maswali manne pekee katika kijitabu cha majibu ulichopewa.
(b) Swali la kwanza ni la lazima.
(c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani:
Tamthilia, Riwaya, Ushairi na Fasihi Simulizi.
(d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
(e) Karatasi hii ina kurasa tano zilizopigwa chapa.
(f) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

Kijitabu hiki kina kurasa 3 ambazo zimepigwa chapa

Fungua ukurasa

SEHEMU A : FASIHI SIMULIZI (alama 20)

1. (a) Ngomezi ni nini? (alama 2)
(b) Taja sifa nne za ngomezi . (alama 4)
(c) Fasihi ya ngoma ina nafasi katika jamii ya sasa. Thibitisha. (alama 14)

SEHEMU YA B:
SWALI 1 : SHAIRI

2. ***Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata.***

1. Subira ni kitu chema, kiumbe ukiwa nayo,
Haraka ina ulema, unapoufata moyo,
Saburi ina salama, kwa sababu waliyonayo,
Laiti ukisubiri, utapoa moyo wako.

2. Subira yalete heri, na mengi mafanikio,
Haraka huleta shari, haraka ina kilio,
Subira hasa ni nzuri, tazama wasubirio,
Laiti ukisubiri, utapoa moyo wako.

3. Subira hata kwa penzi, subirisha wako moyo,
Usijivike kitanzi, japo mapenzi unayo,
Pupa hudhuru mapenzi, kwa kila hali iwayo.
Laiti ukisubiri, utapoa moyo wako.

4. Penzi la sasa utani, sioni wafaidio,
Imebaki nukusani, maovu na mchukio,
Wapendanao huoni, wametua masikio,
Laiti ukisubiri, utapoa moyo wako.

5. Penzi kuliendekeza, litakupa usumbuo,
Utashindwa kufanyiza, kazi ya kupata nguo,
Penzi lije kukulaza, na ukose mzinduo,
Laiti ukisubiri, utapoa moyo wako

6. Ukiendea shindo, penzi bila kuzuio,
Litakuchezesha kondo, uwape cheko wenzio,
Pendo hilo silo pendo, bali ni masingizio,
Laiti ukisubiri, utapoa moyo wako.

7. Nimewaona azizi, wakiwa na mali zao,
Hufukuzwa kama mbuzi, na hao hawapendao,
Heri kuvaa kitanzi, moyo upate kikao,
Laiti ukisubiri, utapoa moyo wako.

8. Pendo lisikuhadai, kukupa tabu ya moyo,
Na wewe ukajidai, ukadanganyika kwayo,
Usione kukurai, utakuja kulia yoyo.
Laiti ukisubiri, utapoa moyo wako.

(a) Taja hasara nne za utovu wa subira zilizoangaziwa katika beti tatu za kwanza. (alama 4)
(b) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
(c) Onyesha idhini ya mshairi katika shairi. (alama 3)
(d) Andika ubeti wa sita kwa lugha ya nathari. (alama 4)
(e) Dhihirisha mitindo miwili tofauti ya matumizi ya uradidi katika shairi hili. (alama 2)
(f) Fafanua maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi hili. (alama 3)
(i) Lisikuhadai
(ii) Azizi
(iii) Nuksani

SEHEMU YA C: TAMTHILIA
Kithaka wa Mberia: Kifo Kisimani.

Jibu swali la 3 au 4

3. "Ujeuri, mwenzangu ni kidonda-kitiliwe dawa."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Kando na mzungumziwa taja na ueleze wahusika wengine waliotawaliwa na ujeuri na jinsi ulivyowaathiri. (alama 6)
(c) Eleza namna mwanamke alivyosawiriwa katika tamthilia ya Kifo Kiismani. (alama 10)

4. Kwa kutolea mifano eleza mbinu zifuatazo zilivyotumika katika tamthilia ya Kifo Kisimani. (alama 20)
(a) Jazanda
(b) Chuku
(c) Ndoto
(e) Mbinu rejeshi

SEHEMU YA D: RIWAYA YA UTENGANO
Said A. Mohammed

FASIHI
UTENGANO

5. "Ibilisi wa mtu ni mtu." Dhibitisha ukweli wa methali hii kwa kurejelea riwaya ya Utengano. (alama 20)

6. "Furaha ilikuja baadaye ingawa itakuwa si furaha kitu, maana damu yake itakuwa imeshapotea …….
Aliona itakuwa faraja kulipa kisa kwa mkasa , faraja kubwa kuutua mzigo wa madhila, ……..
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 3)
(b) Ni damu ya nani iliyopotea na ilipoteaje. (alama 6)
(c) Je mzigo wa madhila alitwikwa na nani na ameutuaje? (alama 7)
(d) Taja na utolee mifano mbinu zilizotumika katika dondoo hili. (alama 4)

SEHEMU YA E: HADITHI FUPI
K.W. Wamitila: Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingie.

Mkimbizi (John Habwe)

7. (a) Jadili athari za vita katika haditi hii. (alama 12)
(b) Jadili umuhimu wa wahusika wafuatao.
(i) Mzee Savalanga
(ii) Msimulizi (alama 8)

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
JULAI, 2011

MTIHANI WA SHULE ZA UPILI WA KUJITAYARISHIA KCSE, WILAYA YA MAKINDU
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI LA 3
LUGHA

MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

SEHEMU A : FASIHI SIMULIZI (alama 20)

1. LAZIMA

(a) Ngomezi ni nini? Ngomezi ni sanaa na ngoma (alama 2)

(b) Taja sifa nne za ngomezi (alama 4)

(i) Hushirikisha matumizi ya zana za muziki.
(ii) Wana jamii huweza kuufasiri mdundo wa ngoma
(iii) Ujumbe mzito maalum na wa dharura huweza kuwasilishwa kwa njia nyepesi au rahisi na isiyo ghali.
(iv) Ujumbe unaowasilishwa huweza kufichwa kwa wasiohusika.

(c) Fasihi ya ngoma ina nafasi katika jamii ya sasa. Thibitisha. (alama 14)

(i) Ambulensi
(ii) Kengele katika magorofa
(iii) Simu za rununu huwa na toni mbalimbali.
(iv) Shuleni shughuli hudhibitiwa na kengele.
(v) Kanisani na mahakamani.

Majibu – shairi

2. (a) Hasara

- Kulemaa
- Shari
- Kilio
- Hudhuru mapenzi (alama 4)

(b) Umbo

- Mizani 8, 8 – 16 kila mshororo
- Kibwagizo. Laiti ukisubiri utapoa moyo wako.
- Beti ni 8.
- Vipande viwili – ukwapi - utao
- Vina vinabadilikabadilika
- Kila ubeti una mishororo minne – Tarbia

Kijitabu hiki kina kurasa 5 ambazo zimepigwa chapa

Fungua ukurasa

(c) Idhini

- Kuboronga sarufi mf. Subirisha wako moyo, na mengi
- Inkisari – unapoufata
- Tabdila – usumbuo, lisikuhadai, tabu

(d) Ubeti wa sita – nathari

Ukifanya mapenzi bila kadri na kipimo utaaibika na kuishia kuchekwa na marafiki .
Mapenzi ya aina hiyo si mapenzi halisi mbali ni urafiki au kujifanya . Afadhali usubiri ili moyo wako utulie.
Hakiki kazi ya mtahiniwa uthibitishe kuwa pana mtiririko wa kihathari na mawazo yote yamewakilishwa.

(e) Mitindo miwili ya uradidi

Matumizi ya neno subira katika ubeti wa 1, 2 na 3 au neno penzi katika ubeti 4, 5 na 6.
Matumizi ya fungu / kibwagizo (uradidi wa fungu)
Kilichorudiwa mwishoni wa kila ubeti n.k.

(f) Maana ya maneno

(i) Lisikudanganye / hisikuhangaishe / lisikusumbue.
(ii) Penzi / mwandani.
(iii) Nuksani – kisirani / usumbufu/ kero.

SEHEMU YA C : TAMTHILIA

Kithaka wa Mberia : Kifo Kisimani . Jibu swali la 3 au 4

3. "Ujeuri, mwenzangu ni kidonda-kitilie dawa."
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Kando na mzungumziwa taja na ueleze wahusika wengine waliotawaliwa na ujeuri na jinsi uliyowaathiri. (alama 6)
   (c) Eleza namna mwanamke alivyosawiriwa katika tamthilia ya Kifo Kiismani. (alama 10)

4. (a) Maneno haya yalisemwa na Atega akimwambia askari wa III. Walikuwa nje ya gereza. Atega alikuwa amemwomba Askari III amruhusu kumpa Mwelusi chakula. Askari alimkataza kuwa hangeweza kufanya mambo apendayo. Akawaambia waweke vikapu chini na kuondoka.

   (b) Wahusika wengine waliotawaliwa na ujeuri.

   Bokono

   Anapuuza ushauri wa mkewe kuhusu uogozi mbaya na malalamiko ya raia =athari-aliondolewa uongozini.

   Gege

   Anakataa kumtembelea Mwelusi gerezani ana muua Mwelusi.

   Batu

   Anapanga mashambulizi na kupuuza malalamiko ya raia.
   = athari-alikamatwa na raia na kushtakiwa.

   Andua

   Kuteka maji kisimani kinyume na kanuni za Mtemi.
   - athari – alijeruhiwa usoni.

(c) Sifa za mwanamke

- Ni mlezi bora Tanya
- Ni washauri mfano Nyalwe
- Wanamapinduzi ; Atega, Andua, Tanya, Azena.
- Kama vyombo vya kumstarehemwanaume mfano kisa kuhusu mpenziwe Bikono.
- Wenye busara Nyalwe aliweza kutambua kuwa mumewe anasumbuliwa na kitu Fulani. Tanya anatambua mpango wa Batu anapokuwa akimtafua Mwelusi.
- Ni wadaku- uhusiano kati ya Atega na Mwelusi.
- Ni jasiri: - Nyalwe, Atinga, Andua

Kifo Kisimani

Kwa kutolea mifano eleza jinsi mbinu zifuatazo zilivyotumika katika tamthilia ya Kifo Kisimani.

(a) Jazanda

Kozi na njiwa – Batu na Nyalwe
Macho ya Butangi – Washauri
Miguu ya Butangi
Mwiba
Chatu
Jiwe
Kibanda
Jua
Mkate wa wishwa

(b) Chuku

- Bokono kuongoza kwa miaka mia moja
- Viuno vitayeyuka
- Urembo wa Alida

(c) Ndoto

Ndoto ya Bokono – alizikwa hai
Ndoto ya Tanya kuhusu samba aliyejeuliwa kisimani

(d) Mbinu rejeshi

- Kisa cha Makea
- Askari wa II walivyomuua mtuhumiwa
- Mawazo ya Mwelusi – kuhusu hali ilivyokuwa Butangi kabla

Swali 3 Muktadha

(a) (i) Haya ni maelezo ya mwandishi kumhusu Farashuu.
(ii) Alipoelezwa namna Maksuudi alivyoghadhabika aliporudi kwake.
(iii) Walipomtorosha Maimuna

(alama 3)

(b) (i) Damu ya Mwanasururu aliyekuwa ameolewa na Maksuudi iliyopotea.
(ii) Kifo chake kinatokana na mateso ya kunyang'anywa mali kijanja na kwa kutumia nguvu.
(iii) Maksuudi alizoea kumpiga Mwanasururu hadi kuzimia.
(iv) Mwanasururu alighafilika anakunywa pombe na kuwa mlevi, alianza uhuni na kutembea ovyoovyo.
(v) Alipata mtoto nje ya ndoa na baadaye alipatwa na wazimu.
(vi) Alisababisha (Mwanasururu) mwanawe Kabi kugongwa na gari na kupoteza mguu wake mmoja.

6 x 1 = 6

(c) (i) Aliyemtwika Farashuu mzigo wa madhila ni Maksuudi.
(ii) Uchungu wa kupoteza mwanawe ulikuwa mkali kiasi cha kutaka kulipiza kisasi.
(iii) Alishirikiana na Mashoga wake Kazija na Biti Kocho kulipiza kisasi.
(iv) Kazija alikuwa na urafiki na Mussa mwanawe Maksuudi na kutumia fursa hii kuwafumanisha kutenganisha Mussa na Maksuudi.
(v) Biti Kocho alimshawishi Maimuna waandamane hadi Madongoporomoka na njiani kumtonesha kidonda cha kutawishwa nyumbani.
(vi) Alitumia mwanya uliotokea wa Bi. Tamima kushikwa na uchungu na kutaka usaidizi wa Mkunga.
(vii) Alizungumza na Maimuna na kukubaliana amfuate baadaye amsaidie kutoka kwao.

UTENGANO

4. - Adui wa mtu ni mtu.
- Kazija vs Maksuudi
- Farashuu vs Maksuudi
- Maksuudi vs – Musa
  - Maimuna
  - Tamima
  - Kitoto
  - Mwanasururu
- Biti Sururu => wasichana => makahaba
- Mama Jeni => Maimuna, Dora na makahaba
- Kazija => Musa
- Farashuu => Maimuna / Tamima
- Biti Kocho => Maimuna
  => Tamima
- Shoka vs Selume
- Maksuudi => Wananchi
  => Wafanyakazi
- Zanga => wananchi
- Maksuudi => Fadhili
- Makahaba => wenyewe kwa wenyewe

Zozote 10 x 2 (utoe maelezo)

SEHEMU YA E : HADITHI FUPI
K.W. Wamitila: Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine.

Mkimbizi (John Habwe)

7. (a) Jadili athari za vita katika hadithi hii. (alama 12)
(i) Vifo vya watu wengi.
(ii) Uharibifu wa mali ya thamani
(iii) Kukatizwa kwa elimu
(iv) Magonjwa
(v) Ukosefu wa lishe bora
(vi) Uyatima
(vii) Kusambaratika kwa familia n.k

(b) Jadili umuhimu wa wahusika wafuatao

(i) Mzee Savalanga

- Mzee mwenye hekima
- Alipoteza jamaa yake akiwa mdogo kwa sababu ya vita
- Mwenye utu na huruma
- Alimshauri Msimulizi ili aanze kurudi na kuielimisha jamii yake
- Hakuona haja ya vita vya kikabila.

(ii) Msimulizi

- Mhusika mkuu
- Alitamani kusoma ili aisaidie jamii yake.
- Anaonyesha kuipenda nchi yake kwani alitamani kurudi kwao.
- Ndiye nguzo muhimu ya kuonyesha haja ya kuondoa ukabila ambao unaweza kuleta madhara makubwa katika jamii.

(alama 8)